# Siasa, Uchumi na Ustawi wa Jamii: Mtazamo wa Kisemiotiki wa Ushairi wa Kivumba

*Sanja, L. W. Leo*[1], *Kitula King'ei*[1] na *Richard Wafula*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Nairobi*
[2]*Chuo Kikuu cha Kenyatta*

**Ikisiri**

**Makala hii inachunguza nafasi ya ushairi katika kuzungumzia masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni pamoja na ustawi wa jamii kupitia ushairi wa Kivumba. Ili kukuza mjadala wetu, makala hii ilifafanua ishara na maana katika ushairi wa Kivumba kwa kutumia nadharia ya semiotiki kutumia misimbo ya Barthes. Lengo la mjadala wetu ni kubainisha ya kwamba, ushairi unaweza kuwa chombo mbadala cha kuzungumzia masuala yanayoikumba jamii kikamilifu. Makala hii inazingatia kauli kwamba, malighafi makuu ya fasihi simulizi ni jamii. Makala hii inajadili kwamba, sio rahisi kufasiri ishara na maana katika ushairi wa jamii yoyote nje ya mkutadha wa jamii yenyewe. Ili kuongoza mjadala huu, mjadala ulijikita katika ushairi wa Kivumba pekee kwa kutumia misimbo mitano ya Barthes. Ushahidi wote uliotegemewa katika mjadala wetu ni ule uliotokana na mifano iliyokusanywa kutoka nyanjani katika maeneo ambapo Kivumba kinazungumzwa nchini Kenya baina ya 1919-2020.**

**Maneno Muhumu:** Ushairi, Siasa, Uchumi, Ustawi, Kivumba, Semiotiki, Kiishara, Kirejelezi

**Utangulizi na Mapitio ya Maandishi**

Dhima ya ushairi wa Kiswahili ni kuzungumzia masuala yanayoikumba jamii kwa kutumia lugha yenye mnato (Mlamali, 1980). Ujumbe na mbinu ya uwasilishaji hufungamana katika kufanikisha mawasiliano. Mbinu hizo hufumbata maana nasibishi inayowasilishwa kupitia ushairi husika. Vitanzu vya fasihi simulizi huwa na lengo la kudhihirisha hisia na maono ya wanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanayowakumba. Malighafi makuu ya fasihi simulizi ni jamii (Senkoro, 1982). Senkoro anaelekea kujadili kuwa, sio rahisi kufasiri ishara na maana ya ishara za kifasihi nje ya muktadha wa jamii husika.

Mjadala katika makala hii ni juhudi za utafiti wa nyanjani uliofanywa baina ya 2019 na 2020. Wahojiwa walikuwa wasemaji asilia wa lahaja ya Kivumba katika maeneo makuu matatu: Wasini, Shimoni na Vanga katika mazingira yao asilia. Mazingira asilia ya Kivumba yalihitajika kwa sababu ufasiri wa maana za ishara aghalabu hutegemea mazoea ya wanajamii husika kulingana na misimbo ya Barthes. Kama wanavyoshadidia Wamitila (2003) na Wellek na Warren (1949), fasihi huashiria ukweli kwa njia ya kutumia ishara za lugha kwa njia ya ubunifu ili kumulika masuala ya kijamii. Namna wanajamii hufasiri maana kutokana na ishara husika hutokana na mazoea na tajriba ya jamii husika ya muda mrefu (Wamitila, 2003). Fasihi simulizi ina mfungamano na maisha ya kila siku ya wanajamii na huonyesha tajriba yao ya kila siku (Wamitila, 2003). Fasihi simulizi na hasa ushairi huwa na dhima ya kuizindua jamii kuhusu uhalisia wa maisha (Iribemwangi, 2013).

Lahaja ya Kivumba ni kongwe na imekuwepo tangu jadi na imekuwa ikitumiwa kutunga ushairi wa Kiswahili kwa kipindi kirefu (Chiraghdin na Mnyampala, 1977; Amana, 1982). Ushairi umetajwa kama sanaa kongwe katika lahaja ya Kivumba na umekuwa ukitumiwa na washairi mbalimbali katika utunzi wa mashairi kwenye fasihi ya Kiswahili (*Malenga wa Vumba,* 1982). Katika utangulizi wa diwani ya *Malenga wa Vumba,* Msami anatoa kauli ya kwamba, ushairi wa Kivumba ni sanaa ya jadi. Tunanukuu:

> Kwa kawaida, Wavumba ni washairi wa kale na asili na Lugha yao ya Kivumba hupendeza mno ikitumika katika mashairi ya Kiswahili na huweza kumsaidia sana mshairi kwa kufupiza mizani na kurefusha. (*Malenga wa Vumba,* 1982:1-8)

Kulingana na dondoo, Wavumba walikuwa wakitumia ushairi kama chombo cha mawasiliano tangu jadi. Msami anafichua taswira tatu kuhusu fasihi simulizi ya Kivumba: mashairi katika lahaja ya Kivumba ni sanaa ya kongwe. Aidha, washairi wa Kiswahili wamekuwa wakitumia lahaja ya Kiswahili katika utunzi wa mashairi na kutoa mchango muhimu kwa ustawi wa mashairi ya Kiswahili kimuundo na kiutanzu. Amana basi amedhihirisha ya kwamba, fasihi simulizi ya Kivumba ina uwezo wa kuzungumzia masuala ibuka katika fasihi ya Kiswahili katika diwani yake. Ametumia lahaja hiyo katika mashairi kama: *Kiwiliwili sikia* (uk. 24) na *w-a-s-i-f-u-w-a B-a-b-a-K-e-n-y-a-t-t-a* (uk. 66). Mashairi hayo yanabainisha hali ya kijamii na kisiasa (*kiwiliwili sikia*) na (*wasifuwa baba Kenyatta*) ya jamii hii. Kwa kuwa mtunzi anatumia msamiati wa Kivumba, inachukuliwa kwamba mashairi yake yalihusu Wavumba pia.

Mwingine aliyegusia ushairi wa Kivumba ni Lambert. Lambert alikusanya ushairi wa Kivumba ambao kwa manufaa ya utafiti wetu, tumeuita; *Wimbo wa Mwanahamisi* (Lambert, 1962 na 1965). Tunanukuu:

*Rwaa vyombovyo, rwaa, Makame ya Makame!*
*Ndiwe jakamoyo, ndiwe chimbamoyo!*
*Nirendeje, mume wangu?*
*Kwende na umbea-umbea.*
*Mri, kuyongoya mri!*

**Tafsiri**
Twaa vyombo vyako, twaa Makame wa Makame
Wewe ni ndiwe tatizo, ndiwe kero la moyo wangu
Nimtendea vipi mume wangu?
Nenda na umbeaumbea wako (ufuska wako)!
Mti hupepea kama mti
(Lambert, 1962: 14-18) (Tafsiri ni yetu)

Kulingana na dondoo, Makame wa Makame alikuwa ni mzinzi. Lambert anatoa maelezo kuwa, ‘chimbamoyo,’ ni msamiati wa Kivumba wenye maana ya kitamathali.Tamathali hiyo inayorejelea mhusika mwenye tabia ya kifuska. Wavumba waliheshimu asasi ya ndoa na usafi wake na hiyo ndiyo maana nasibishi ya tamathali hiyo. Ilikuwa juu ya mwanamke katika jamii hii kuidumisha ndoa yake.

Mckay alishughulikia ushairi wa Kivumba pamoja na mapisi (Mckay, 1975). Mtagusano kati ya Warabu na Wavumba ulivuruga maisha yao kijamii na kisiasa. Washirazi ndio waliangusha ngome ya utawala wa Wavumba katika eneo la Vumba Kuu. Chiraghdin na Mnyampala (1977) pamoja na Amana (1982) wananukuu shairi kuhusu tukio hilo. Tunanukuu:

*Tata litatile tata, litatile gunge*
*Uje wembe wa kupata, na noo la muiringo*
*Rutenge rukalikata, hata matata yatenge*
*Nyumba inaing’ia tenge, Mwanenaje mawaria?*

Kulingana na dondoo, kuanguka kwa Vumba Kuu kulisambaratisha jamii ya Kivumba kisiasa na kijamii. Kuanguka kwa Vumba Kuu kuliwafanya Wavumba kutawanyikia katika mengine kama Wasini, Shimoni na Vanga. Shairi hilo linatumia ishara ya ‘nyumba’ kuwasilisha maana nasibishi ya kwamba, jamii nzima ya Kivumba iliathirika. Mabadiliko ya kiwakati huathiri maudhui na lugha kifasihi (Shariff 1988). Shairi hilo linahusu juhudi za Wavumba za kujijenga upya kama jamii. Ushairi huo ulikuwa basi sauti ya urazini katika jamii ya Kivumba kwa muda mrefu.

McKay anabainisha kufungamana kwa maisha ya kijamii na ya kisiasa ya Kivumba kupitia ushairi wa *Nema*. Tunanukuu:

*Mukanyeni Nema vumba asije chena*

*(Vumba) yaja na mwavuli, jumbe k’ako yaona vema*

**Tafsiri**
*Mkanyeni Nema asije Vumba tena*
*Acha na (amejifunika) Mwavuli, anajua vyema jumbe hayuko (ameaga)*
(Tafsiri ni yetu)

Katika kipindi cha kuomboleza kiongozi, Wavumba hawakufanya kazi, kwenda vitani ama kufanya ugomvi na majirani. Maombolezo yalichukua siku arobaini (McKay, 1975). Katika kipindi hicho, hakuna aliyeruhusiwa kufunika kichwa chake kwa kofia ama nguo kama heshima kwa kiongozi. Tamathali na ishara ya 'mwavuli' inawasilisha maana nasibishi ya kwamba, Neema anawakejeli Wavumba wakati wanaamwomboleza kiongozi wao nahuo ni uchokozi wa kisiasa. McKay anaonyesha kuwepo kwa mshikamano huo zaidi kupitia ushairi wa *Kipitu,* Tunanukuu:

*Kipitu ya mwakoroyo simwoga*
*Sende mwona ziwani yakoga*
*Akambia "namkiamke kisuga"*
*Nimwole "mwana maere na ruga"*

**Tafsiri**
Kipitu mwana wa Mwakoroya sio mwoga
Nilimpata akiogelea ziwani, kisha akaniambia, "acha mieleka ianze''
Nikamweleza,"mwana maere na ruga"
*(*Tafsiri ni yetu)

Dondoo linaashiria kuwa, Kipitu anatafuta makabiliano na mshairi. Wavumba walikuwa na itikadi kuhusu masuala kama kifo, utawala, mtoto na mwanamke. Walitumia ngoma kupitisha jumbe kuhusu kifo cha kiongozi. Kulikuwa na sherehe nyingine kama kumtawaza diwani (kiongozi) iliyoitwa. Mke wa diwani alipompata mtoto wa kiume, sherehe hiyo ilirudiwa. Kulikuwa na sherehe nyingine iliyoitwa kumbi la ada. Hii ilihusishwa na tohari ya mtoto wa kiume.

Kwa vile mjadala katika makala hii ulilenga kuweka wazi maana nasibishi zinazowasilishwa kupitia kiitanzu cha ushairi, makala hii iliuchunguza vipengele husika kwa kutumia nadharia ya semiotiki. Semiotiki ni utohozi wa neno la Kiingereza, *semiotics* ambalo vilevile limetoholewa kutoka kwa neno la Kigriki, *semeiotikos* lenye maana ya ufasiri wa ishara. Neno *seme* lina maana ya ishara. Ishara ni kitu chochote ambacho kinawasilisha maana na ambayo sio ishara yenyewe. Kwa mijibu wa semiotiki, hiyo ni maana nasibishi ya ishara. Nadharia ya semiotiki imetumika katika nyanja mbalimbali kama vile: falsafa, isimu, sanaa na fasihi, saikolojia, sanaa ya ujenzi, takwimu, anthropolojia na sosholojia kati ya nyingine.

Barthes ni wa karibuni sana baada ya De Saussure, Peirce na Jakobson. Kazi zake maarufu ni kama: *Writing Degree Zero* (1954) *Mythiologies* (1957), *The Death of the Author and Elements of Semiology* (1964) *The Fashion Systems* (1970), *The Pleasure of the Text* (1973), *S/Z* (1974) na *Lovers Discourse* (1977). Barthes alipendekeza kuweka matini za kifasihi katika vijisehemu vidogovidogo ambavyo aliviita leksia. Leksia hizo zilimwekea msingi wa kilichokuja kujulikana kama misimbo ya usomaji ya Barthes. Barthes alikuza dhana kwamba, kila hadithi hujumuisha zaidi ya msimbo mmoja. Wingi wa misimbo ndiyo humsisimua msomaji wa matini za kifasihi kusoma kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kauli yake inakuza msingi wa msimbo wa matukio na msimbo wa kihemenitiki. Kulingana na Barthes, ili kupata maana husishi na maana nasibishi ya ishara, ni sharti mfasiri wa ishara azingatie uhusiano uliopo baina ya ishara na kiashiriwa. Katika *Mythologies* (1957), Barthes anashadidia suala la kuzingatia mazingira na utamaduni wa kijamii ambamo matini zinazochanganuliwa zimeibukia. Ishara moja inaweza kuwa na maana nasibishi tofauti iwapo ishara hiyo itafasiriwa katika utamaduni tofauti. Hata katika utamaduni mmoja, kuna uwezekano ishara hiyohiyo ikawa na maana tofauti. Kulingana naye, mielekeo maarufu ya kitamaduni mara nyingi ndiyo hutumiwa kufasiri ishara kwa njia inayokubalika na wengi. Barthes anatumia mfano wa ishara ya mvinyo wa Kifaransa kudhihirisha kauli yake. Kulingana naye, tabaka lenye ushawishi huweka mielekeo ya kufuatwa na jamii. Hii ina maana kuwa, ishara inaweza kuwa ileile lakini maana nasibishi zikawa tofauti kutegemea mfasiri wa ishara, dhamira na maarifa ya kijamii alionayo. Mfasiri wa ishara basi anahitaji kutumia hekima yake

mwenyewe pamoja na maarifa ya kijamii kuifasiri ishara inayochanganuliwa. Kauli hiyo ya Barthes inakuwa msingi wa msimbo wa urejelezi.

Katika, *The Fashion System* (1970), Barthes anafafanua ya kwamba, vazi huvaliwa kuashiria sherehe fulani maalum. Suti inaweza kuashiria tukio rasmi. Sherehe ndiyo maana nasibishi ya ishara. Kulingana naye, viwanda hutumia picha na vishawishi kama hivyo kuendelea kuuza fashioni. Kauli hiyo inawekea msingi msimbo wa kiishara na msimbo wa kiseme. Katika kitabu chake *Sur Racine* (1963*)*, Barthes anatazama matini zote kama mfumo wa ishara ambazo zinahitaji ufasiri ili kuibua maana nasibishi. Anapendekeza usomaji horomo wa matini za kifasihi. Katika *S/Z* (1970:17-18), Barthes anahimiza msomaji wa matini kung'amua maana ya ndani ya matini kwa kutumia vielekezi mbalimbali vilivyomo katika matini zenyewe. Kila msimbo ni sauti ambayo imefungamanishwa na matini zinazochunguzwa. Katika *The Pleasure of the Text*, Barthes (1973) anajadili kwamba, hata pale ambapo msomaji wa matini za kifasihi anasoma kwa njia ya kujiburudisha, kuna kiwango ambapo hufika akabaini maana nasibishi ya matini husika. Aliita hali hiyo ung'amuzi huru. Yaani kuna wakati ambapo mfasiri wa ishara hupata maana ambayo iko kando sana na mazoea yaliyopo. Katika usomaji wa aina hiyo, msomaji wa matini anatafuta vielekezi ambavyo vitamwongoza katika kufikia maana ya ishara husika nje ya muktadha uliozoeleka.

Barthes anajadili kuwa, mielekeo ya kijamii huelekeza namna lugha na mtindo wa uandishi hutumiwa kupitia kazi yake ya *Writing Degree Zero (*1953). Muundo wa mwandishi huathiriwa na mielekeo ya kibinafsi na ile ya kijamii. Baadhi ya ishara zinaweza kufasirika tu kwa kupimwa kwenye mizani ya mielekeo iliyopo. Maana za ishara hubadilika kulingana na mabadiliko ya kiwakati pamoja na matarajio ya wanajamii (Barthes, 1973). Pia, baadhi ya ishara hazihitaji ufafanuzi zaidi ya maana husishi ya ishara. Barthes anapendekeza msomaji wa matini za kifasihi kutenganisha matini na mwandishi wake katika, *The Death of the Author* (1968). Tulijadili na kufasiri ishara na maana katika ushairi wa Kivumba kwa kutumia misimbo ya Barthes ya kiishara na kirejelezi. Msimbo wa kiishara unajadili kwamba, kila ishara ina maana husishi na maana nasibishi. Ishara ya kiishara inatambulika kutokana na muktadha na malengo ya matumizi kwani ndio hubainisha iwapo ishara husika ina maana nasibishi au ni husishi (yake) pekee. Ushairi hutumia ishara na tamathali kwa wingi ishara hizo huibua maana nasibishi za aina mbalimbali. Msimbo wa kiishara basi hutumiwa kurejelea mfumo wa ishara ambazo huashiria maana husishi na maana nasibishi za ishara kwa kurejelea muktadha na malengo ya utumizi. Ishara inaweza kuwa ni kitu dhahiri, mazingira ama usemi fulani unaoashiria maana nasibishi. Hivi ni kusema ya kwamba, kila ishara huwa na maana husishi na maana nasibishi na ufasiri hutegemea uwezo wa mfasiri wa ishara wa kutambua maana nasibishi zinazobainishwa na ishara kwa kutumia vigezo vya mkutadha na malengo ya matumizi.

Barthes (1970) anatazama matini zote kama mfumo wa ishara ambazo zinahitaji kufasiriwa ili kuibua maana nasibishi. Kauli yake inahusu msimbo wa kirejelezi ambao huwa na viashirii vya kitamaduni. Kama anavyoshadidia Wamitila, msimbo huu hujengwa kwa misingi ya viashirii vya utamaduni (Wamitila, 2002). Viashirii vya kitamaduni huwa vinafahamika tayari kwa mfasiri wa ishara kutokana na maarifa yake ya muda mrefu ya kijamii mbalimbali aliyonayo. Msimbo wa kirejelezi basi huhusu namna msomaji wa matini za kifasihi huishia kufasiri ishara na kupata maana nasibishi kutokana na tajriba yake ya muda mrefu kutoka katika maarifa ya kijamii (kitamaduni), mielekeo yake ama itikadi zake (Barthes, 1970).

**Mjadala na Matokeo**

Katika kujadili ushairi na ustawi wa jamii kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni kupitia ushairi wa Kivumba kisemiotiki, mjadala wetu utajikita katika ufasiri wa ishara na maana kama ilivyojibainisha katika ushairi mbalimbali wa Kivumba pekee. Ufasiri wa ishara na maana katika ushairi wa Kivumba ulifanywa katika misingi ya vigezo vya matukio ya kimapisi, kijamii na kiuchumi vilivyoashiriwa katika ushairi teule kwa kuongozwa na nadharia ya semiotiki, misimbo ya Barthes ya kiishara na kirejelezi.

**Siasa, Jamii na Utamaduni**

Kulingana na ushairi wa Kivumba, jamii na siasa ni vipengele ambavyo vimefungamana. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) neno siasa lina maana nyingi. Maana mojawapo ni kwamba, siasa ni mfumo wa kuongoza serikali za kitawala. Ni mfumo kwa sababu ndani yake kuna mifumo mingine mingi. Utawala wa Kivumba uliingiliwa na Warabu (Mckay, 1975). Washirazi waliiba *Ngoma Kuu* ya Wavumba. Ngoma ilikuwa mojawapo wa nguzo kuu za utawala wa Kivumba. Washirazi waliwahamisha Wavumba na kuwafanya wakimbilie katika maeneo mengine. Baadhi ya Wavumba walikwenda maeneo ya Tanzania. McKay (1975), Chiraghdin na Mnyampala (1977) pamoja na Amana (1982) wananakili shairi kuhusiana na mgogoro wa Wavumba na Warabu.Kwa manufaa ya utafiti wetu, tumeliita, *Zani Imengia.*

Matumizi ya ishara za '*nyumba*, *wembe*, *kuta*' na '*kujenga*' kuashiria uharibifu ambao jamii ya Kivumba ilipitia katika kipindi cha Washirazi. 'Ngome ya Vanga' ni ishara ya makabiliano kati ya Wavumba na wageni. Eneo la Vanga lilipata jina lake kutokana na uvamizi na wageni. Wavumba walikuwa na makabiliano na wazungu vilevile. '*Vanga*' maana yake kulingana na Kivumba, ni panga; yaani mahali ambapo wenyeji walijihami kwa mapanga dhidi ya wageni. Sauti 'v' katika lahaja ya Kivumba, inatokana na lafudhi ya wenyeji.

**Athari za Kisiasa**

Wavumba waliathirika kisiasa na wageni. Katika shairi la, *Zani Imeingia,* tunanukuu:

1. *Nyumba k'aiezikeke, nyumba madonye-madonye*
*Nyumba k'aingandikiki, nyumba misonge-misonge*
*Nyumba hii ivunjiki, simamani ruijenge*
*Nyumba inaing'ia tenge, mwanenaje, mwawaria?*
(Chiraghdin na Myampala 1977: 35 ubeti wa 2)

Kulingana na dondoo, mshairi anataka wanajamii kuzinduka na kuijenga jamii yao upya. Mshairi anatumia ishara za kiishara na kirejelezi. 'Nyumba' ni ishara ya kiishara. Msimbo wa kiishara hutumiwa kurejelea mfumo wa ishara ambazo huashiria maana husishi na nasibishi ya ishara. Ishara moja inaweza kuwa na maana zaidi ya ishara yenyewe. Maana nasibishi ya ishara ya 'nyumba' kupitia msimbo wa kiishara ni jamii nzima ya Kivumba. Jamii nzima ya Kivumba iliharibiwa kisiasa Washirazi walipovamia ngome yao (McKay, 1975). Jamii hii ilibaki bila mshikamano. Miongoni mwa uharibifu ulioikumba jamii ya Kivumba katika kipindi cha Washirazi ni kuhamishwa kwa wenyeji, kupoteza makazi na maisha kama inavyoashiriwa na: '*Nyumba k'aiezikeke, nyumba madonye-madonye* na '*Nyumba k'aingandikiki, nyumba misonge-misonge'.* Kupitia msimbo huu inadhihirika ya kwamba, Wavumba walifadhaika na kuteseka kisiasa na kijamii. Kisemiotiki, kiashirii kinaweza kuwa kilekile bali kinachorejelewa kikawa kitu tofauti kabisa. '*Nyumba inaing'ia tenge, mwanenaje, mwawaria?'* kiishara ni wito kwa wanajamii kuchukua hatua za kujijenga upya. Katika lahaja ya Kivumba, sauti *t* hutamkwa kama *r*.

Ushairi huu unatumia ishara za kirejelezi vilevile. Kama anavyoshadidia Wamitila (2002), viashirii hivyo vya kitamaduni humwezesha mfasiri wa ishara kuelewa aina ya ishara na maana inayowasilishwa moja kwa moja. Tunanukuu:

2. *Chena sana ruzikaze, hata nyumba ruigange*
*Mbugu ruzik'utanize, yosi ruizonge-zonge*
(Chiraghdin na Myampala 1977: 35 ubeti wa 2)

Kupitia dondoo, inabainika ya kuwa, mshikamano wa jamii ya Kivumba ulivurugwa na kulikuwa na haja ya kuwaleta tena wanajamii pamoja. '*Kuzikaza pande za nyumba'.* Ni ishara ya kirejelezi kwa kuwa kuta za nyumba zinaashiria jamii nzima na kundi la watu pamoja na utamaduni wao. Wavumba popote walipo, wanastahili kurejea mapisi yao na kujiimarisha tena kama jamii. Kupitia kukamilishana kwa misimbo hiyo, maana zinazoibuka ni kwamba, wajibu wa kuijenga upya jamii ya Kivumba ni wa Wavumba wote. Dhima ya ushairi katika jamii hii kuhusu udumishaji wa mapisi na kuhifadhi utamaduni ni bayana katika jamii hii. Katika jamii za Kiswahili, washairi ndio walikuwa sauti ya wanajamii na walikuwa na majukumu ya kuzungumzia masuala yanayowakabili wanajamii

(King'ei 1999). Sanaa ya ushairi ni ya jadi katika jamii hii na ulitumiwa kuhifadhi matukio muhimu ya kimapisi kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo siasa (*Malenga wa Vumba*, 1982).

**Siasa na Miiko ya Kijamii**

Wavumba walikuwa na itikadi za kuomboleza hasa viongozi. Ushairi wa *Nema* unajikita katika dhamira za maombolezo kwani unahusu *kipera* cha sifo. Arege na Matei wanaeleza maghani kama:

> …tungo za kishairi ambazo hutolewa pasi kuimbwa.
> Tungo hizi huwa hazina mahadhi bali hughanwa tu.
> Maghani husimulia hadithi au jambo fulani kwa mapana.
>
> (Arege na Matei, 2005:159)

Kupitia dondoo, maghani ni ushairi simulizi wa kughaniwa tu bali sio wa kuimbwa. Maghani yasio ya kawaida husimulia mapisi ama matukio maalumu (Arege na Matei). Huambatana na ala kama ngoma, maleba kama njuga na sifa nyinginezo. Katika ushairi wa *Nema,* tunanukuu:

3. *Mukanyeni Nema vumba asije chena*
   *Yaja namwavuli, jumbe k'ako yaona vema*

**Tafsiri**

> Mwonyeni Nema asije Vumba tena
> Anakuja na mwavuli ilhali anafahamu jumbe hayuko tena
> (Kutoka McKay, 1975. Tafsiri ni yetu)

Kulingana na dondoo, Nema amekuja kuwakejeli Wavumba wakati wamo kwenye maombolezo ya kiongozi wao. Wavumba wanapokuwa kwenye maombolezi ya kiongozi wao, hawakufanya kazi ama kuvaa kofia (McKay 1975). Kifo na maombolezo ni matukio ya kijamii na kitamaduni na yanaweza kufasiriwa tu kwa kutumia maarifa na tajariba ya kijamii na ndiposa tendo linalorejelewa ni la kirejelezi. Kupitia msimbo huu basi tunapata maana nasibishi ya kwamba, kiongozi wa Kivumba anapoaga, Wavumba waliomboleza kwa siku arobaini kulingana na desturi za jamii hii kama inavyoashiriwa na: '*jumbe hayuko tena'.* Kupitia msimbo huu maana nasibishi nyingine inayobainika ni kwamba, Wavumba wanapinga wanaokiuka miiko na itikadi zao pamoja na hisia zao za kisiasa. Kimapisi, Wavumba walikumbana na ugomvi kati yao na majirani zao kama Wachichifundi, Wadigo pamoja na wageni kama Warabu (McKay 1975). Hayo yanathibitishwa kupitia ushairi wa *Kipitu* (Anwani ni yetu). Katika ushairi wa *Kipitu*, tunanukuu:

4. *Kipitu ya mwakoroyo simwoga*
   *Sende mwona ziwani yakoga*
   *Akambia "namkiamke kisuga"*
   *Nimwole "mwana maere na ruga" (*McKay, 1975:272-3)

**Tafsiri:**

> Kipitu mwa wa Mwakaroyo si mwoga
> Nilimkuta akiogelea ziwani
> Akanileza, "Acha mieleka ianze"
> Nimwone, "Mwana mkorofi huleta janga kwao" (Tafsiri ni yetu)

Kwa mujibu wa dondoo, Kipitu anawachokoza Wavumba kwa kuvunja mwiko wa kujinadhifisha wakati kiongozi wa jamii hii ameaga dunia. Kulingana na msimbo wa kirejelezi, ishara za kitamaduni huwa zinaeleweka na mfasiri wa ishara tayari. 'Kuongelea mtoni' ni ishara ya kirejelezi kwa sababu inahusu utamaduni wa Kivumba nyakati za kuomboleza. Ilikuwa ni kinyume cha mila za Kivumba mwanajamii yeyote kujinadhifisha katika siku arobaini za kuomboleza kiongozi (Hollis, 1900; McKay, 1975). *"Nimwole "mwana maere na ruga"*: *Mwana mkorofi huleta janga kwao*. Maana nasibishi ya kauli hiyo kwa kutumia msimbo wa kirejelezi ni kwamba, Wavumba walikuwa tayari kulinda hadhi yao ya kisiasa pamoja na desturi zao. Wavumba wakati wanamwomboleza kiongozi, walifuata desturi maalum. Mojawapo ni kuwa, walikuwa hawajinadhifishi wala kubadilisha mavazi. Kipitu kwa hivyo alikuwa anawachochea Wavumba kwa makabiliano. Msichana wa Kivumba

alipoolewa, hakutarajiwa kurejea nyumbani kwao kwa maana atawatia aibu watu wa kwao. Maana nasibishi ni kuwa, kisiasa, Wavumba hawakuogopa vita vya kisiasa.

**Uchumi na Ustawi wa Jamii**

Kamusi ya Karne ya 21 toleo la (2011) inaeleza uchumi kama njia za uzalishaji mali; biashara. Mashairi ya Kivumba yakifasiriwa kwa kutumia misimbo ya Barthes ya kirejelezi na kiishara, yanabainisha dhamira mbalimbali kuhusu hali za kiuchumi za Wavumba. Katika *S/Z*, Barthes anahimiza msomaji wa matini kung'amua maana nasibishi za ishara kwa kutumia vielekezi mbalimbali vilivyomo katika matini zenyewe. Kulingana na Barthes, kila msimbo ni sauti ambayo imefungamanishwa na matini zinazochunguzwa (Barthes, 1970). Hii ina maana ya kwamba, ishara moja inaweza kuashiria maana nasibishi zaidi ya moja kutegemea dhamira, muktadha na maarifa ya kijamii ambamo inaibukia. Misimbo ya Barthes ya kiishara na kirejelezi inatumia misingi hiyo katika ufasiri wa ishara katika matini za kifasihi kuhusu maana za kiuchumi.

**Uvuvi**

Shughuli kuu za kiuchumi za Wavumba ni wavuvi. Katika Shairi la, *Wasini,* tunanukuu:

5. *Kazi zetu za Wasini, niza mashaka*
*Mpaka tuende baharini, ndio mke atapika*
*Au yaje majapari, kisite kuyapeleka*
*Mji wetu wa Wasini ni mji wenye baraka*

Kupitia dondoo ni kwamba, kutokana na ukosefu wa kazi na njia mbadala za kiuchumi, Wavumba walitegemea uvuvi ili kujipatia riziki kwa muda mrefu kufikia sasa. Katika, *The Fashion System* (1970), Barthes anafafanua ya kwamba, vazi huvaliwa kuashiria sherehe fulani maalum. Sherehe basi ni maana nasibishi ya vazi. Hii ina maana ya kwamba, maana husishi ya ishara huwa ni kielelezo cha maana nasibishi ya ishara. Maelezo yake yanapanua namna msimbo wa ki-ishara na namna ambavyo huwa unatumiwa. '*Mpaka tuende baharini, ndio mke atapika.*' '*Kazi zetu za wasini, ni za mashaka*' ni ishara za kiishara kwa sababu zinazoibua maana nasibishi za ishara. Wavumba walitegemea uvuvi kwa sababu hawana njia mbadala za kujipatia riziki.

Kwa mujibu wa msimbo wa kirejelezi, mfasiri wa ishara anaweza kutambua moja kwa moja aina ya ishara anapoihusisha na dhamira na muktadha. '*…ni mji wenye baraka*' ni ishara ya kirejelezi kwani kinaibua maana nasibishi kuhusu masikitiko ya jamii hii dhidi ya hali yao ya kiuchumi. Kibwagizo husika ni kirejelezi cha hali ya kutamaukiwa kwa Wavumba kiuchumi.

**Raslimali**

Wavumba hawana raslimali nyingi za kuwawezesha kustawi haraka kiuchumi. Katika shairi la, *Wasini*, tunanukuu:

6. *Maji yetu ya mabirika, mara nyingi hukauka*
*Yakiisha twenda Shimoni, kuyapata ni mashaka*
*Au yaletwe na meli, yana kutu na taka*
*Mji wetu wa Wasini ni mji wenye baraka (*Tafsiri ni yetu) (Ubeti wa 4)

Dondoo linaeleza kuwa, Wavumba walikabiliwa na ukosefu wa raslimali za kimsingi kama kukosa maji safi ya kunywa. Mazingira yao kwa ujumla ni magumu hasa wanaoishi katika kisiwa cha Wasini kwani hata usaafiri na kupata bidhaa muhimu ni ghali na mara nyingi hupata huduma mbovu. Kwa mujibu wa msimbo wa kiishara, kila ishara huwa na maana husishi na maana nasibishi. *'Maji yetu ya mabirika, mara nyingi hukauka, Yakiisha twenda Shimoni, kuyapata ni mashaka,* ni mishororo inayotumia ishara za kiishara maana 'kukauka' na 'kuendea Shimoni' ni ishara zinazobainisha uhalisi kwamba, Wavumba hawana visima vya maji safi na hasa Wasini. Vanga kuna kisima kimoja pekee. Maana ya ndani ni kuwa, wanajamii wengi wa Kivumba wanaishi katika mazingira magumu.

**Uozo wa Kijamii**

Ukosefu wa raslimali umesababisha kuibuka kwa tabia hasi miongoni mwa wanajamii. Katika shairi la, *Vya Kuokota*, tunanukuu:

7. *Waroro wanalirera, zumbwiridera nyumbani*
*Wanena walirokora, huko Masulini*
*Kupenda sana kuphara, kalirwaa mwafulani*
*Uchaphara kitu gani, kwa vitu vya kurokora?*

Dondoo linatoa ujumbe kwamba, watoto katika jamii hii wanatumia njia za udanganyifu kuiba samaki wa mwenyewe (raslimali za wenyewe) kutoka kwenye kidimbwi (makazi ya wenyewe) kwa sababu ni tabia ambayo wanaiona katika watu wazima. Kulingana na msimbo wa kiishara, ili kupata maana husishi na maana nasibishi ya ishara, ni sharti msomaji wa matini za kifasihi azingatie uhusiano uliopo baina ya ishara na kiashiriwa. '*Samaki'* ni kiisharia cha raslimali ya aina yoyote ile katika jamii ya Kivumba. Kupitia msimbo huu basi ni kwamba, baadhi ya wawanajamii wa Kivumba wameshindwa kuwapa watoto wao maadili kutokana na hali ngumu ya maisha. Maana nasibishi ya ndani ni kuwa, uvivu umechangangia katika uibukaji wa tabia hasi miongoni mwa Wavumba.

Kulingana na msimbo wa kirejelezi, mfasiri wa ishara hujenga uhalisia maalumu katika fikra zake kutokana na ishara inayochunguzwa kutokana na viashirii vya kitamaduni. Viashirii hivyo vya kitamaduni humwezesha mfasiri wa ishara kuelewa aina ya ishara na maana inayowasilishwa moja kwa moja. *'Uchaphara kitu gani, kwa vitu vya kurokora?'* ni ishara za kirejelezi kinachoonyesha kudhoofika kwa maadili ya baadhi ya wanajamii wa Kivumba. Katika shairi la, *Wasini*, tunanukuu:

8. *Kaditema kituoni, kalama phwachi naikaa*
*Kisiwa kyeru zamani, pombe haramu kufika*
*Hivi sasa olani, wanarurerea mgokaa*
*Mji weru wa Wasini ni mji wenye baraka*

Kulingana na dondoo, wanajamii wameingilia uraibu mbaya wa kupotosha katika jamii hii kama kunywa '*pombe*' na kula '*mgokaa*'. Kulingana na dondoo, haya ni mabadiliko ambayo yamesababishwa na mapito ya wakati. Msimbo wa kirejelezi hujengwa kwa misingi ya viashirii vya utamaduni kwani ufasiri wa ishara za aina hizo huelekezwa na mazingira ya kitamaduni kutokana na tajriba aliyonayo ya kijamii. *'Pombe haramu' na 'mgokaa'* ni ishara za kirejelezi zenye maana nasibishi kuhusu tabia ngeni katika jamii ya Kivumba. Jamii ya Kivumba imeanza kukengeuka kutokana na kutagusana na mazingira ya wanajamii wengine. Hizo pia ni ishara za kiishiria kwani kwa mujibu wa msimbo wa kiishara, ishara inaweza kuwa ileile lakini maana nasibishi zikawa tofauti kutegemea mfasiri wa ishara na dhamira ya kufanya hivyo. Kuna maana nasibishi ya kwamba, Wavumba wamekengeushwa.

**Thamani ya Kufanya Kazi**

Wavumba wanahimiza kufanya kazi ili kumfaidi mtu binafsi pamoja na jamii. Katika wimbo wa *Wajenzi*. Tunanukuu:

9. *Ukawakute mchana shughuli zina wajaa*
*Wafanya yenye maana kama vile mashujaa*

*Nyuki ni wachanga sana kundi moja*
*Wanawake kwa hali ya kupatana*
*Wamejenga ujamaa.x 2*
*Ukawakute mchana shughuli zina wajaa*
*Wafanya yenye maana kama vile mashujaa*

*Nyuki uvivu hawana wajihadhari na njaa*
*Kazi zao dana dana waruka na kuramkaa*
*Mzinga ukajazana mara asali yajaa*
*Kumrera mrina kuja kuirwaa.* X2

Kulingana na dondoo, nyuki hufanya kazi kama jamii na ndiposa wanafaulu. 'Nyuki' ni ishara ya kirejelezi kulingana na msimbo wa Barthes. Wavumba wanathamini mshikamano hata katika kazi. Kamusi ya Karne ya 21 toleo la *(*2011) inaeleza utamaduni kama mila, desturi, asili ama jadi ya jamii fulani. Utamaduni basi ni namna jamii fulani ya watu inavyoishi maisha yao na masuala wanayoyathamini kama jamii.

**Thamani ya Ndoa**

Ndoa katika jamii ya Kivumba ni tukio la kijamii. Katika wimbo, *Nguo* (*Anwani ni yetu*), tunanukuu:

10. *Makameah nguo yangu mbovu*
*Kwaitia vumbi sefuu eeh*
*Tukavue nyavu maji yajaa*
*Linaanza linaanza x2 goma*
*La mkugo kina mama rusikae*
*Eeh kando kando ujooni rulicheza weeh goma hilo*
*Naona umejifunga vibwe vibwe*
*Sasa kwaphwera cheza ndombolo ndombolo x2*

Kulingana na dondoo hili, Wavumba wanathamini asasi ya ndoa. Ni wakati ambapo mwanamume wa Kivumba anatarajiwa kumnunulia mkewe nguo ya harusi: '*Tukavue nyavu maji yajaa'.* Kulingana na msimbo wa kirejelezi, ishara za kitamaduni huwa zinaeleweka na mfasiri wa ishara tayari. Sherehe yenyewe ni tukio la kijamii tayari na linaweza tu kufasiriwa kwa kutumia msimbo wa kirejelezi. Harusi huwa ni wakati wa jamii nzima na hasa kina mama wa Kivumba kujumuika pamoja. Ishara ya 'Nguo', mwito kwa 'wanawake kuingia kwenye sherehe' na kucheza 'ndombolo' ni ishara za kirejelezi ambazo zinaashiria kutimia kwa ndoa katika jamii hii. Ishara za kitamaduni huwa zinaeleweka na mfasiri wa ishara tayari na hujenga uhalisia maalumu katika fikra za mfasiri wa ishara. Densi ya 'ndombolo' hata hivyo sio utamaduni wa Kivumba. Huu ni mtindo wa densi maarufu iliyoanzia huko DRC na huhusisha kuchezesha kiuno kwa nguvu na kimviringo. Huchezwa baina ya wanaume na wanawake. Kulingana na msimbo wa kirejelezi basi, jamii ya Kivumva imeathirika kutokana na tamaduni za kimataifa. Msimbo wa ki-ishara unasema kuwa, ishara inaweza kuwa ni kitu dhahiri kama umbo la kitu, mazingira ama usemi fulani. Hiyo ndiyo maana nasibishi ya kiishara ya: *Kwaitia vumbi sefuu eeh: Waitia vumbi…'* Nguo na vumbi inaashiria aibu ambayo mwanamke katika jamii hii anakuwa nayo iwapo atakosa kuhudhuria sherehe ya harusi na pia kukosa kanga mpya.

**Wosia wa Kindoa kwa Wasichana**

Wanawake wa Kivumba walipewa mawaidha kuhusu kuishi katika ndoa. Katika shairi la *Ndoa* (T.H.J) tunasoma:

11. *Mume ni mosi wa kuni, usiphoaka hufuka*
*Sue jitia uhuni, mume achakubanduka*
*Umjue aphwerani, moyowe uchakunjuka*
*Ndoa yamlazimu, kwa wosi wanadamu*
*(*W. 6 Ubeti wa 4: Kutoka nyanjani*)*

**Tafsiri**

Mume ni moshi wa kuni, usipowaka hufuka
Bora usijitie uhuni, mume atakubanduka
Umjulie ataka nini, roho yake itafunguka
Ndoa inamlazimu, kwa kila mwanadamu

Kulingana na dondoo, mwanamke katika jamii hii alistahili kuwa mnyenyekevu na mwenye upendo kwa mumewe kama njia ya kudumisha ndoa. Hata hivyo, hatuoni masharti kama hayo kuhusu wanaume. Wasichana katika jamii ya Kiswahili walifundwa kulingana na utamaduni (Chiraghdin 1974). Kulingana na msimbo wa kiishara, ili kutambua aina ya ishara, mfasiri wa ishara anastahili kutathmini muktadha na dhima ya ishara husika katika kuwasilisha maana nasibishi inayowakilishwa. 'Kuni' na 'moshi' ni ishara za kiishara ambazo zinaibua maana nasibishi kuwa, mwanamume katika

jamii hii ndiye kichwa cha familia. Hii ndio maana nasibishi inayoshiriwa na: 'Mume *ni moshi wa kuni, usipowaka hufuka.'* Maana nasibishi ya ndani ni kuwa, mwanamume wa Kivumba hata awe mnyonge, anabaki kuwa kiongozi wa nyumba na mwanamke katika jamii hii anastahili kumtii: *Bora usijitie uhuni, mume atakubanduka.* 'Kujitia uhuni' ni ishara ya kiashiria inayoonyesha kiburi ambacho mwanamke katika jamii hii na anatahadharishwa kukiepuka. Ishara hizo: '*moshi wa kuni, usipowaka hufuka'* pia ni za kirejelezi zenye maana nasibishi ya kwamba, jamii ya Kivumba ilimwandaa mwanamke kwa ndoa kwa sababu jamii hii hairuhusu talaka. Hiyo ndio maana nasibishi ya '*…atakubanduka.'*

**Uadilifu Katika Ndoa**

Wavumba hawaruhusu ufuska katika asasi ya ndoa. Katika ushairi wa *Mwanahamisi,* tunanukuu:

12. *Rwaa vyombovyo, rwaa, Makame ya Makame!*
*Ndiwe jakamoyo, ndiwe chimbamoyo!*
*Nirendeje, mume wangu? Kwende na umbea-umbea.*
*Mri, kuyongoya mri!" (Lambert 1962: 14-18)*

**Tafsiri**

Twaa vyombo vyako, twaa, Makame wa Makame
Wewe ndiye tatizo, ndiwe wanikera moyoni
Nimtendeeje mume wangu? Nenda na hila-hila (zako)
Mti hupepea kama mti!"

Kulingana na dondoo, Makame ni mzinzi na anafukuzwa kwa sababu anataka kuzini na mke wa mwenzake. Msimbo wa kirejelezi unasema ya kwamba, ishara za kitamaduni huwa zinaeleweka na mfasiri wa ishara tayari. Hali inayorejelewa ni ya kirejelezi kwa sababu uzinzi ni tukio linalohusiana na suala la kijamii na tamaduni za mahusiano kindoa. Mwanamke wa Kivumba ana dhima ya kudumisha ndoa yake: '*Nimtendeeje mume wangu?* Wajibu mkubwa wa kindoa katika jamii hii umeachiwa mwanamke zaidi na sio mwanamume ambaye ndiye kichwa cha jamii. Mwanamke wa Kivumba basi amedhibitiwa zaidi kuliko mwanamume.

Msimbo wa kiishara huhusu namna mfasiri wa ishara katika huunda maana husishi ya ishara katika fikra zake na jinsi maana hiyo humwongoza kwenye maana nasibishi ya ishara. Maana nasibishi inaweza kutokana na majukumu ya ishara husika ama viashiria vyake vingine katika matini. '*Mri, kuyongoya mri! Mti hupepea kama mti!"* ni ishara za kiishara. Katika jamii ya Kivumba, mwanamwali anatarajiwa kujitunza miiko ya ndoa kabla kuolewa. '*Mti kupepea kama mti'* ni ishara ya kiishara inaibua maana nasibishi ya kuwa, wanajamii wa Kivumba wanatarajiwa kuwa na maadili na kufuata taratibu za jamii hii.

**Wajibu wa Malezi na Ukungwi**

Wajibu wa mzazi na kungwi katika jamii ya Kivumba kwa mtoto wa kike ni dhahiri. Katika wimbo wa, *Arusi,* tunanukuu:

13. *Kina mama karuphwere shari ruli wa kanyaa*
*Na barua rokawareea zao usalama*
*Koma mama jitu zima kuruwaadama*
*Koma salaaa mwana*
*Wakuuphi walioranguilia na hivi sasa*
*Na hivi sasa runakwisha waingilia aaah*
*Lia mwana kulia wenda kiona kiboksi mayoya*
*Ruwaingia aaah aaah leo ruwaingia aah x2*
*Wakuwuphi waliorungulia na hivi sasa*
*Rwaingia na bibi harusi rwaingia aah*

Kulingana na dondoo, malezi ya mtoto msichana na maandalizi yake hadi ametimiza umri wa kufunga ndoa ni wajibu wa mama ama kungwi. Sherehe ya harusi ni ishara ya kirejelezi kwa sababu

ukungwi ni ishara ambayo inaweza kufasiriwa tu kwa kutegemea elimu za kijamii na kitamaduni. Mama mazazi na kungwi katika jamii hii alistahili kuhakikisha ya kuwa, mwanamwali anapata mafunzo mema na kujilinda hadi siku ya kuozwa. Msimbo wa kiishara hutumiwa kurejelea mfumo wa ishara ambazo huashiria maana husishi ya ishara na maana nasibishi. Kupitia msimbo huu tunapata maana nasibishi kuwa, mwanamke wa Kivumba huandaliwa kisaikolojia na kungwi kuhusu ndoa mapema kama inavyoashiriwa na: '*Lia mwana kulia wenda kiona kiboksi mayoya'.* Sherehe ya harusi huwa pia kipindi cha kuwasuta wale ambao walikuwa na shaka kuhusu uwezo wa mama mzazi na kungwi: *'Na barua rokawareea zao usalama',* na *'Wakuuphi walioranguilia na hivi sasa.* Hata hivyo, inaonekana ni mwanamke katika jamii hii pekee ndiye ameachiwa wajibu huo muhimu: *Wakuwuphi waliorungulia na hivi sasa: wapo wapi waliotuingilia na sasa hivi.*

**Malezi ya Mtoto**

Wavumba wanathamini malezi ya watoto. Bembezi ni nyimbo za kuwabembeleza watoto ili walale (Wamitila 2004). Katika bembezi ya, *Mwana,* tunanukuu:

14. *Ooowah owaah mroro x2*
*Owaah owaah mroro maponda*
*Mamayo kenda mjini kafunga pisi mbili za mpunga.*
*Mwana mizi mrere rumpigie utete akija*
*Mama atete akija baba atete*
*Ukalia waniliza wanikumbusha ukiwa*
*Ukiwa wa baba na mama*
*Naphwera kiphepheo ni ubwabwa wa mwana umroro*

Kwa mujibu wa dondoo, mlezi ana wajibu wa kumfundisha mtoto na kumwelekeza kuhusu adabu njema na maadili. Kulingana na msimbo wakirejelezi, viashirii vya kitamaduni huwa vimetapakaa ndani ya matini zinazochanganuliwa. Basi ishara: '*Owaah owaah mroro maponda, Mamayo kenda mjini kafunga pisi mbili za mpunga:* Yaani: *Owaah owaah mwana mashavu na mamayo amekwenda mjini kuleta punje mbili za mpunga'* ni ishara za kirejelezi kuhusu namna malezi ya mtoto yanavyochukuliwa katika jamii ya Kivumba. Mtoto anathaminiwa katika jamii hii na wajibu mkubwa wa kulea ni wa mwanamke (mlezi). Barthes katika *The Pleasure of the Text* (1975) anapendekeza ufasiri horomo wa ishara katika matini. Katika ufasiri wa aina hiyo, mfasiri wa ishara hutafuta ishara ambazo zitamwongoza katika kufikia ufasiri wa maana nasibishi ambazo zinaashiriwa na ishara. Kupitia msimbo wa kiishara, '*mbegu mbili za mpunga'* zinaashiria maana husishi ya kibaba cha mtoto. Hata hivyo, maana nasibishi ya ishara husika ni kwamba, mwanamke katika jamii hii alitakiwa kumlisha mtoto.

**Mabadiliko katika Ndoa**

Hali ya kiuchumi na kijamii imebadilisha ndoa katika jamii ya Kivumba. Katika shairi la, *Wasini,* tunanukuu:

15. *Wanawake wa zamani, sasa wanageuka*
*Kwa kaa majumbani, hata kwenye mabinka*
*Sasa wende madukani, bila hata kujifinika*
*Mji weru wa Wasini ni mji wenye Baraka*

Kwa mujibu wa dondoo, wanawake wa kisasa wamebadilika na sio kama wale wa zamani kwa sababu kwa sasa mwanamke hasalii nyumbani bali anatoka na kwenda kutafuta riziki kama mwanamume. Vile vile hawafuati taratibu za kujistiri wanapokuwa katika hadhara. Kisemiotiki, baadhi ya ishara zinaweza kufasirika tu kwa kupimwa kwenye mizani ya mielekeo iliopo (Barthes, 1972). Kauli hii inashadidia msimbo wa kiishara. Ishara moja inaweza kuwa na maana nasibishi kwa kutegemea muktadha wa wakati. Kwenda bila 'kujifunika' ni ishara ya kiashiria ambayo inaonyesha kubadilika kwa tabia miongoni mwa wanawake katika jamii hii. Maana nasibishi ya ndani ni kwamba, mwanamke katika jamii hii sasa amekuwa huru zaidi kutokana na kujikomboa kiuchumi. Ushairi huo ukifasiriwa na msimbo wa kirejelezi unaibua maana nasibishi ya kuwa, mwanamume wa Kivumba

ameanza kupoteza nafasi yake kama kichwa cha familia: '*Wanawake wa zamani, sasa wanageuka'.* Maana nasibishi ya ndani ni kuwa, kwa sababu ya mabadiliko katika asasi ya ndoa, maadili ya kijamii hii yameanza kuathirika. Mabadiliko katika asasi ya ndoa katika jamii hii yanatokea mijini na hata pamoja na vijijini. Katika shairi la *Ndoa,* tunanukuu:

16. *Kuphara majaaliwa, nakuomba usijeumbuka*
*Runao walo mjini, wao kawalibahatika*
*Na sitara ya mwilini, daima rwawakumbuka*
*Ndoa ya mlazimu, kwa wosi wanadamu*

Sio kila mwanajamii katika jamii hii yuko katika ndoa. Hali hasa ni mbaya zaidi mijini (mishororo wa 1 na 2). Kulingana na msimbo wa kirejelezi, viashirii vya kitamaduni humwezesha mfasiri wa ishara kuelewa aina ya ishara na maana nasibishi inayowasilishwa kwa kutumia vielekezi vilivyomo katika mazingira husika kama inavyoashiriwa na:*'Runao walo mjini, wao kawalibahatika'* ni kirejelezi kinachoonyesha mabadiliko yanayotokana na utamaduni mpya unaosababishwa na kuibuka kwa miji: '*Runao walo mjini,wao kawalibahatika': Tunao mumu humu mjini, ambao hawakubahatika'.*

**Kitovu cha Lugha na Utamaduni**

Kitovu cha lugha na utamaduni wa Kivumba ni miji yao. Miji kama Wasini, Shimoni na Vanga kwa sasa ndio kitovu cha utamaduni wa Kivumba hasa baada ya kuanguka kwa Vumba Kuu (McKay 1975, Hollis 1900) Katika shairi la *Wasini,* tunanukuu:

17. *Mji weru wa wasini, ni mji wenye baraka*
*Tokea hiyo zamani, kina baba kina kaka*
*Wala sineni utani nane kwa hakika.*
*Mji weru wa wasini ni mji wenye baraka*.

Kulingana na dondoo, miji ya Wavumba kama Wasini ni ya kijadi. Kisemiotiki, baadhi ya ishara zinaweza kufasiriwa tu kwa kupimwa kwenye mizani ya mielekeo iliopo katika jamii. *'Tokea hiyo zamani, kina baba kina kaka,'* ni ishara yakirejelezi kwani inatumia viashirii vya kitamaduni. Inaibua maana nasibishi kuwa, utamaduni wa Kivumba unafungamanishwa na historia na vilevile na mazingira yao. Mazingira hayo yanahusu miji na maeneo ambako Wavumba wanapatikana na lugha yao inazungumzwa kiasili. Maana nyingine ya Kivumba kulingana na wahojiwa ni 'kucheza ngoma' yaani, *wa-* ni kiambishi kinachorejelea wanajamii wa Kivumba –watu wanaocheza ngoma. Katika *Writing Degree Zero (*1953), Barthes anajadili kuwa, mielekeo ya kijamii huelekeza namna lugha na mtindo hutumika. Barthes ana maana kuwa, ufasiri wa maana nasibishi ya ishara hutegemea matumizi ya wengi katika jamii. Yaani, wanajamii ndio hubainisha muktadha na maana nasibishi inayowasilishwa kupitia ishara inayochunguzwa. Wasini ni kati ya miji inayohusishwa na lahaja ya Kivumba. Katika shairi la, *Kilio cha Kivumba*, tunanukuu:

18. *Kwanza ujuwe miamba, vizuri uchachokowa*
*Nayakukokora kwamba, mashazi ruyachukuwa*
*Mayaru yawe ya ng'amba, uokoke na vikowa*
*Kivumba kwakichafuwa, rwalalamika wavumba*

Kwa mujibu wa dondoo, ili kufahamu utamaduni wa Kivumba, ni sharti kujifunza kwanza mila na desturi zao kikamilifu. Kulingana na Barthes, ishara huwa na maana ya kijuuju na maana ya ndani (Barthes 1970). '*Kujua miamba'* na '*viatu vya kutumia*' ni ishara ya kiashiria inayoibua maana nasibishi ya kwamba, wageni wanastahili kujifundisha desturi za Kivumba: '…*kujua miamba*'. Wavumba wanahimiza wageni kujifundisha mila na utamaduni wao badala ya kutumia kiburi ama nguvu kwa kizingizio cha usomi.

**Thamani ya Lugha na Utamaduni**

Wavumba wanathamini lugha na utamaduni wao. Katika shairi la, *Kilio cha Kivumba,* (*Taz: kiambatisho 13)* tunasoma:

19. *Ndimi kongwe la Kivumba, kauze uchaambiwa*
*Siyo lugha ya kuomba, n' lugha nilovyaliwa*
*Siye yule mwajigamba, namwira mwaruchafuwa*
*Kivumba kwakichafuwa, rwalalamika Wavumba*

Kwa mujibu wa dondoo, lahaja ya Kivumba ni kongwe na ina wasemaje wake ambao ni Wavumba. Ubeti huu unahusu msimbo wa kirejelezi kwa kuwa, lugha ni sehemu ya utamaduni wa watu (Iribemwangi na Mukhwana, 2011). Tajriba ya muda mrefu ya mfasiri wa ishara katika maarifa ya kijamii ni muhimu kwani ndio humwezesha mfasiri wa ishara kung'amua maana nasibishi ya ishara: '*Siyo lugha ya kuomba, ni lugha nilozaliwa nayo'* Maana nasibishi ya ndani inayoibuliwa na msimbo huu ni kuwa, *Kivumba* ni kitambulisho cha wanajamii hawa cha kwanza: '*... kaulize utaambiwa'*. Kulingana na msimbo wa kiishara, njia moja ya kupata maana nasibishi ni kutazama majukumu ya ishara husika. '*Siyo lugha ya kuomba, n' lugha nilovyaliwa'* ni taashira ya kiishara. Wavumba hasa wazee wanathamini lugha na utamaduni wao. Kizazi kikongwe cha Kivumba kinapinga kuvurugwa kwa utamaduni wao na wageni. McKay ananakili ya kwamba, aliwasikia wazazi wa Kivumba wakiwahimiza watoto wao kujivunia utamaduni na lugha yao na kuepuka ukengeushi (McKay, 1975). Tunanukuu: "*Nilisikia wazazi wakiwaeleza wana wao, wewe sio Mwarabu bali Mvumba."* Wavumba walitakiwa kujiepusha na ukengeushi miongoni kutoka nje na badala yake kuthamini utamaduni wao.

Kauli ya McKay inashadidiwa na sensa ya mwaka wa 2019. Idadi ya Wavumba ni watu 1,449 pekee. Katika utangulizi wa, *Malenga wa Kivumba* (1982:1-4), Msami anashadidia kauli ya mshairi kuhusiana na mila na desturi za Kivumba. Amana alitumia lakabu, 'Malenga wa Vumba' kwa sababu maalum. Tunanukuu:

> Boukheit wavyele wake wa upande wa kuukeni nao vilevile ni Waswahili wenye asili ya wenyeji wa…Vumba. Boukheit aliweza kuupata vizuri ulimi mtamu wa Kivumba, lugha ambayo kwake ni ulimi wa mama… (Amana, 1982:2)

Kulingana na dondoo, Amana alijinasibisha na Wavumba kwa sababu mama yake ni Mvumba. Athari za kigeni hata hivyo zimeleta mabadiliko katika jamii ya Kivumba na hasa kwa vijana. Katika shairi la *Kilio cha Kivumba, tunanukuu*:

20. *Kweru karuli komba, rumuonapho rwaawa*
*Kwakuomba wajichimba, kikweru kukiumbuwa*
*Kivumba kwakichafuwa, rwalalamika Wavumba*
(W. 13 ubeti wa 4)

Kwa mujibu wa dondoo, Wavumba hawana desturi ya kuiga tabia za kigeni kiholela na hasa zenye itikadi mbovu. Hali hiyo inatumia ishara za kirejelezi na ishara za kiashiria '*kula komba*'. Viashirii hivyo vya kitamaduni humwezesha mfasiri wa ishara kuelewa aina ya ishara na maana nasibishi inayowasilishwa moja kwa moja. Ishara ya 'komba' ni ya kirejelezi kwa sababu inarejelea utamaduni mgeni ambao umeathiri jamii ya Kivumba na kuvuruga amali zao. Mabadiliko ya kiwakati yameanza kuathiri mfumo wa kiutamaduni wa Wavumba kijamii. '*Komba*' basi ni ishara inayorejelea kitu chochote ambacho kinakwenda kinyume na utamaduni wa Kivumba kisemiotiki kulingana na msimbo wa kirejelezi.

**Hitimisho**

Kupitia mjadala wetu, imebainika ya kuwa, siasa, uchumi, jamii na utamaduni ni asasi ambazo zimefungamana pamoja na ustawi wa jamii yoyote unategemea mshikamano wa hizo asasi. Katika jamii hii, ndoa ni ngome ya mwanamke ingawa mwanamume ndiye kichwa cha nyumba. Hata hivyo, kuna mabadiliko katika asasi hii yanayoletwa na mabadiliko ya kiuchumi na mtagusano na tamaduni za kigeni. Mwanamke katika jamii hii anazidi kuwa huru zaidi na nafasi ya mwanamume inaanza kutishiwa. Uzinzi na talaka inapingwa katika jamii hii. Aidha, Wavumba wanathamini malezi ya watoto. Kiuchumi, jamii hii haina raslimali nyingi. Shughuli muhimu za kiuchumi za Wavumba ni uvuvi. Sehemu nyingi hazina raslimali kama maji safi ya kunywa. Pia, miundomisingi katika jamii hii ni duni. Usafiri kutoka kisiwani Wasini na maeneo mengine ya Kivumba unategemea mashua.

Kisiasa, Washirazi ndio waliangusha utawala wa Wavumba. Wavumba walilazimishwa kuhamia katika maeneo mengine kama Vanga, Shimoni, Wasini na sehemu za Tanzania.

**Marejeleo**


Abdulaziz, B. H. (1979). *Muyaka: Nineteenth Century Swahili PopularScholar Poetry.* Nairobi. Kenye Literature Bureau.

Abedi, K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Dar es Salaam. Eagle Press.

Akaranga, S. D.I. (1987). *Semi za Kiswahili: Maana na Matumizi*. Nairobi. Oxford University Press.

Amana, B. (1982). *Malenga wa Vumba*. Nairobi. Oxford University Press.

Arege, T & Matei, A. (2005). *Kunga za Kiswahili 3: Kitabu cha Mwanafunzi*. Nairobi. Focus Publishers.

Barthes, R. (1974). S/Z. (R. Miller, Trans.) United Kingdom. Blackwell Publishing Ltd.

Barthes, R. (1964). *Elements of Semiology*. New York. Hill and Wang.

Barthes, R. (1968). *Elements of Semiology.*1st Editon. New York. Hill and Wang. (2016*)<https://monoskop.org/images/2/2c/Barthes_Roland_Elements_of_Semiology_1977.pdf*>.

Barthes, R. (1957). *Mythologies.* New York. Hill & Wang.

Barthes, R. (1967). *Elements of Semiology* (trans. Annette Lavers & Colin Smith). Jonathan Cape.

Barthes, R .(1977). Image-Music-Text. S. Heath (ed). *The Journal of Aesthetics and Criticism.* (Vol. 37), (pp. 220.) Hill and Wang.

Barthes, R. (1981). "Theory of the Text" Ian Macleod (Trans), katika R. Young (mh). *Untying the Text.* London. Routledge.

Barry, P. (2002). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory.* Manchester. Manchester University Press.

Chiraghdin, S & Mnyampala, M. (1977). *Hisitoria ya Kiswahili.* Nairobi. Oxford University Press.

Chiraghdin, S. (1974) "Kiswahili na Wenyewe" Katika *Mulika* 6. Kur.35-41.

Hollis, A.C (1900). "Notes on the History of Vumba." *East Africa journal of the Anthropology Institute of Great Britain and Irelanda.* (Pg.275-298).

Kingei, G. K & Kisovi, C.N M (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Lambert, H. E. (1957). *Ki-Vumba, a Dialect of the Southern Kenya Coast.* Kampala: East African Swahili Committee, Makerere College. (uk. 101).

Lambert, H. E. (1958). *Chichifundi: Adialect of Southern Kenya Coast*. Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Lambert, H. E. (1962). *Utenzi wa Vita vya Uhud*. Haji Chum, (ed) (trans). Nairobi. Johari za Kiswahili, (Vol. 3).

Lambert, H. E. (1965*). "*Some Intiation Songs of the Southern Coast*",* Swahili, 35/1. (Uk. 49-67).

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry.* London. Longman Group Limited.

Leech G. N & Short, M. (2007). *Style in Fiction.* London: Pearson Education Limited.

Longhorn Publishers (2012). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi. Longhorn Publishers.

Mckay, W. F. (1975). *"Pre-colonial history of the Southern Kenyan Coast".* Unpublished PhD, Dissertation. Boston University.

Mlacha, S.A.K & Hurskainen, A. (1995). *Lugha,Utamaduni na fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Dar es Salaam. TUKI.

Mlamali, M (1980). *Inkishafi.* Nairobi. Longman Kenya Ltd.

Ndanu, P. & King'ei, G. (1989). *Kamusi ya Methali*. Nairobi. EAEP.

Senkoro, F. M. K. (1984). *Fasihi.* Dar es Salaam. Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia naTahakiki.* Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.

Shariff, N. I. (1988). *Tungo Zetu:* Msingi wa Mashairi na Tungo Nyinginezo. Trenton. The Sea Press, Inc.

TUKI (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam. TUKI.

Wamitila, K .W. (2002 b). *Kamusi ya Misemo na Nahau*. Lulu za Lugha1. Nairobi. Longhorn Publishers.

Wamitila, K .W (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipera Vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Wamitila, K .W (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publishers.

Wamitila, K .W (2004). *Chemchemi za Kiswahili, Kidato cha Tatu*. Nairobi. Longhorn Publishers Ltd.